TASAF yatoa 52.3bn/- kuimarisha muungano

NA ASIA MWALIM

ZAIDI ya shilingi bilioni 52.3 zimetolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) kwa mwaka 2020 hadi 2025, kwa wananchi wa maeneo mbali mbali ya Zanzibar ili kunufaika na fursa za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mratibu wa mpango wa kunusuru kaya masikini Zanzibar, Makame Ali Haji, aliyasema katika ziara ya kuwatembelea baadhi ya wanufaika wa mpango huo, ikiwa ni maadhimisho ya kutimia miaka 61 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema fedha hizo zimetolewa kwa zaidi ya kaya 56,442 za Unguja na Pemba, kwa lengo la kuwainua wananchi kiuchumi kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini.

Aidha alisema maendeleo ya utekelezaji wa miradi ya TASASF, ni juhudi za Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ambao wanaendelea kuudumisha Muungano na kusimamia fursa za Muungano huo kwa pande zote.

Alifahamisha kuwa mpango huo kwa Zanzibar unatekelezwa kupitia vipengele vinne, ikiwemo uhaulishaji wa fedha, ujenzi wa miradi ya miundombinu ya elimu na afya, miradi ya ajira za muda na kukuza uchumi wa kaya kupitia vikundi vya kueka hakiba.

Alisema kupitia kipengele cha ruzuku ya uzalishaji takribani shilingi bilioni 9.8 zimetolewa kwa kaya 24,435 kwa vikundi na wananchi mmoja mmoja wanaozalisha miradi mbali mbali.

Akizungumzia kipenge cha ruzuku ya masharti ya elimu, kutoka mwaka 2020 hadi 2025, alisema takriban wanafunzi 209 wamejiunga na vyuo vikuu kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini kwa Unguja na Pemba.

Kwa upande wa utekelezaji wa ajira za muda alisema miradi 711 imetekelezwa kupitia sekta ya misitu, maji na barabara jambo ambalo limesaidia wananchi kutatua changamoto na kukuza uchumi wao.

Kupitia kipengele cha ujenzi wa miundombinu alisema, zaidi ya bilioni 4 zimetumika katika miradi ya miundo mbinu kupitia sekta ya afya na elimu ikiwemo ujenzi wa madarasa na vituo vya afya ili kutengeneza raslimali watu.

Baadhi ya Wanafunzi walionufaika katika mpango wa kunusuru kaya masikini, Ilham Ali Abdallah, kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), alisema bila ya kupata usaidizi wa TASAF angekosa fursa ya kuendelea na masomo ya juu.

Naye Mtumwa Ali Hija mwafunzi wa SUZA, alisema kutokana na wazazi wake kukosa uwezo bila shaka ingekuwa vigumu kuendelea na masomo katika ngazi ya Chuo Kikuu.

Baadhi ya wananchi walionufaika katika mpango wa kunusu kaya masikini, Khadija Sleyum Saeh (45) mkaazi wa Mwera, mama mwenye watoto saba, alisema fedha zinazotolewa na TASAF zinamsaidia kutimiza mahitaji ya familia yake.